**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**632** **SAYANSI**

**Muda: Saa 3.** **Year: 2023**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Bainisha mifano minne ya magonjwa yanayoenea kwa haraka na kuathiri watu wengi ndani ya muda mfupi.

2. Chambua kwa ufupi hatua nne utakazozitumia kutoa msaada kwa mtu aliyekunywa sumu.

3. Fafanua kwa ufupi mazingira manne yasiyo hai ambayo ni muhimu kwa viumbe hai.

4. Chora sakiti mfuatano kuonesha mpangilio wa amita, voltimita, balbu na swichi.

5. Bainisha matokeo ya mapambano ya kikemikali katika hali zifuatazo:
   (a) Asidi ikidondokea kwenye metali.
   (b) Potasiamu ikichanganywa kwenye bika yenye maji.
   (c) Magneziamu ikiunguzwa kabisa.
   (d) Haidrokloriki asidi ikiwekwa kwenye bika yenye baikaboneti ya sodiamu.

6. Bainisha vifaa vinne vinavyotumika kurahisisha kazi vilivyopo katika kundi la kabari.

7. Eleza kwa ufupi kazi za homoni nne katika hatua za makuzi ya mwili wa binadamu.

8. Chambua mbinu nne ambazo zinaweza kutumika kupunguza ajali katika chumba cha maabara ili kuifanya maabara ya Sayansi iwe sehemu salama ya kujifunzia.

9. Fafanua kwa ufupi taarifa nne muhimu zilizopo katika jedwali la utahini zinazomwongoza mwalimu katika utunzi wa mtihani wa somo lake.

10. Fafanua kwa ufupi zana nne zinazoweza kutumika kufundisha tofauti iliyopo kati ya mimea ya kundi la monokotiledoni na daikotiledoni.

## SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. (a) Chora mchoro wa gurudumu na ekseli, kisha kuonesha sehemu tatu za mchoro huo na
    (b) Kukokotoa
    (i) Uwiano wa mwendo dhahiri,
    (ii) Manufaa ya kimakanika,
    (iii) Jitihada inayotakiwa kupandisha mzigo kwenye gurudumu na ekseli kwa kutumia data ulizopewa: ufanisi wa mashine = 90%, mzigo = 10,000N, urefu wa gurudumu = sm 80, nusu kipenyo cha ekseli = sm 5.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

12. Pendekeza kanuni sita za kufuata ili kupunguza kasi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI katika shule yake.

13. Eleza vigezo vitano vya kuzingatia unapochambua muhtasari wa somo la Sayansi kwa shule za msingi.

14. Tumia hoja sita kueleza umuhimu wa ufundishaji kiduchu kwa wanachuo.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org